

Namna ya kutayarisha Mbolea ya maji

Mbolea ya maji ni chakula cha mimea kilichotayarishwa kutokana na kinyesi cha wanyama

Kinyesi cha wanyama kina virutubisho kwaajili ya mimea.
Lakini kuweka kinyesi cha wanyama moja kwa moja huitunguza mimea!
Mbolea ya maji huilisha mimea salama.

Mbolea ya maji

- Ni bure
- Ni rahisi kutayarisha
- Huongeza mavuno

Huwa tayari ndani ya
siku 7

Tumia kopo moja la mbolea ya maji iliyozimuliwa kwa kila mmea kabla ya kutoa maua kila baada ya wiki 2



Mahitaji

- Samadi mbichi: m.f. Ng'ombe, kuku, mbuzi au sungura
- Chombo: m.f. dumu, pipa, ndoo au chungu
- Kiroba au gunia : m.f. kiroba cha mkaa
- Kamba
- Fimbo
- Maji

Tumia kwenye mboga mboga kama kabichi, nyanya na mahindi

①



Kuweka samadi

Weka samadi kwenye kiroba hodi kufika nusu. Weka jiwe ili kukizamisha.

②



Kufunga kiroba

Funga kiroba na kamba. Kisha fungia kwenye kwenye fimbo.

③



Kuweka kwenye maji

Ingiza kiroba kwenye chombo. Jaza maji kwenye chombo.

④



Kufunika

Funika chombo na kiweka kwenye kivuli ili kuzuua samadi isikimbile hewani.

⑤



Koroga kila siku

Kila siku funua chombo na tikisa kiroba. Mbolea itakuwa tayari baada ya wiki moja.

⑥



Zimua

Ongeza kopo 2 za maji kwa kila kopo moja la mbolea ya maji na tumia ndani ya siku 14.

Sihitaji mbolea za viwandani, ninatumia mbolea ya maji.